# SHERIA YA KUIDHINISHA MAKISIO NA MATUMIZI YA SHILINGI TRILIONI MBILI, BILIONI MIA NANE NA AROBAINI, MILIONI MIA NANE NA HAMSINI NA TATU, LAKI SABA NA THELATHINI NA MBILI ELFU KUTOKA MFUKO MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA SIKU YA TAREHE THELATHINI JUNI, MWAKA WA ELFU MBILI NA ISHIRINI NA NNE NA KURUHUSU UTOAJI NA UHAULISHAJI WA FEDHA HIZO PAMOJA NA MAMBO YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


| VIFUNGU | MAELEZO |
|---|---|
| 1. | Jina fupi. |
| 2. | Tafsiri. |
| 3. | Utoaji wa Shilingi 2,840,853,732,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. |
| 4. | Uwezo wa Waziri kukopa. |
| 5. | Uwezo wa Waziri kwa maombi ya bajeti ya ziada. |
| 6. | Marejesho ya mkopo na riba. |
| 7. | Kukubaliwa kwa Fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. |
| 8. | Mfuko wa pamoja wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. |

JADWELI

**SHERIA NAM. 2 YA 2023**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

23 JUNI, **2023**

# SHERIA YA KUIDHINISHA MAKISIO NA MATUMIZI YA SHILINGI TRILIONI MBILI, BILIONI MIA NANE NA AROBAINI, MILIONI MIA NANE NA HAMSINI NA TATU, LAKI SABA NA THELATHINI NA MBILI ELFU KUTOKA MFUKO MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA SIKU YA TAREHE THELATHINI JUNI, MWAKA WA ELFU MBILI NA ISHIRINI NA NNE NA KURUHUSU UTOAJI NA UHAULISHAJI WA FEDHA HIZO PAMOJA NA MAMBO YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Jina fupi.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Makisio na Matumizi, 2023.

Tafsiri.

**2.** Tafsiri ya maneno yaliyotumika katika Sheria hii, yatakuwa na maana kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016.

Utoaji wa Shilingi 2,840,853, 732,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

**3.** Hazina ya Serikali inaweza kutoa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Nane na Arobaini, Milioni Mia Nane na Hamsini na Tatu, Laki Saba na Thelathini na Mbili Elfu kwa ajili ya matumizi ya huduma kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2024, ambapo Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Nane na Ishirini na Mbili, Milioni Mia Nane na Hamsini na Tatu, Laki Saba na Thelathini na Mbili Elfu kwa ajili ya matumizi ya Serikali Kuu na Shilingi Bilioni Kumi na Nane kwa matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Uwezo wa Waziri kukopa.

**4.**-(1) Waziri anayehusika na fedha anaweza, wakati wowote sio zaidi ya tarehe 30 Juni, 2024, kukopa ndani au nje ya Zanzibar kiasi chochote cha fedha kisichozidi jumla ya kiasi kilichotolewa au kinachochukuliwa kuwa kimetolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali chini ya masharti ya kifungu cha 3 cha Sheria hii kwa njia ya mkopo, mkopo wa awali, mkopo wa hati fungani wa muda mfupi, mkopo wa hati fungani wa muda mrefu au kukopa ziada kupitia hesabu za benki kwa vigezo na masharti kama Waziri atakavyoona inafaa na anaweza kuweka rehani mkopo au ziada katika mali yoyote ya Zanzibar ikijumuisha dhamana ambazo ni sehemu za Mfuko Mkuu wa Serikali.

(2) Fedha zilizokopwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitawekwa katika akaunti ya hazina na zitakuwa sehemu ya Mfuko Mkuu wa Serikali.

(3) Fedha zilizokopwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitalipwa kwa mujibu wa vigezo na masharti yaliyokubaliwa na fedha zitakazohitajika kulipa riba ya mkopo zitatolewa na kulipwa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

(4) Uwezo aliopewa Waziri chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utakuwa ni uwezo wa ziada wa Waziri aliopewa chini ya masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

Uwezo wa Waziri kwa maombi ya bajeti ya ziada.

**5.**-(1) Endapo Waziri anayehusika na fedha amejiridhisha kwamba ni muhimu kwa maslahi ya umma, kutoa matumizi ya ziada kwa wizara au idara yoyote ya Serikali ikiwa ni zaidi ya fedha zilizokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa au huduma ambazo fedha zake hazijaidhinishwa na itakuwa ni hasara kwa maslahi ya umma kughairisha matumizi mpaka pale zitakapotolewa na Baraza la Wawakilishi, bila ya kujali masharti ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote, anaweza kuidhinisha ziada katika fungu lolote lililoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

(2) Endapo Waziri ataidhinisha ziada chini ya kifungu hiki, haraka iwezekanavyo baada ya uidhinishaji huo, atasababisha kuwasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi taarifa ya uhamishaji wa makadirio ya matumizi ya ziada kama hali itakavyokuwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 106 (2) cha Katiba ya Zanzibar, 1984 ikiwa uhamishaji huo utapelekea matumizi ya ziada.

(3) Waziri anaweza kukasimu uwezo wake aliopewa chini ya kifungu hiki kwa afisa yeyote wa umma kwa mujibu wa vigezo na masharti kama atakavyoainisha.

Marejesho ya mkopo na riba.

**6.** Kiasi cha fedha kitakachohitajika wakati wowote kwa ajili ya urejeshaji wa mkopo na riba kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni Shilingi Bilioni Tisini na Mbili na zitalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

Kukubaliwa kwa Fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya kazi za kawaida na miradi ya maendeleo.

**7.**-(1) Fedha zilizotolewa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii, zinaidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo na zitatumika kwa madhumuni na kwa kiwango kilichoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

(2) Makisio ya bajeti kwa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa programu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yataainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

Mfuko wa pamoja wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**8.** Kiasi cha Shilingi Milioni Mia Mbili Arobaini na Laki Tisa zilizotolewa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii, zinaidhinishwa kutoka Mfuko wa Pamoja wa Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**JADWELI**

# JADWELI

## MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| | Wizara/Taasisi | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| **A01** | ***Ofisi ya Rais Ikulu*** | **6,600.1** | 3,964.1 | 0.0 | 0.00 | ***10,564.2*** | 3,400.0 | 0.0 | 0.0 | ***3,400.0*** | ***13,964.2*** |
| A0101 | Kusimamia Huduma na Kuratibu Shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu | 4,362.7 | 1,615.7 | 0.0 | 0.00 | ***5,978.3*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***5,978.3*** |
| A0102 | Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na wazanzibar Wanaoishi Nje ya Nchi | 216.4 | 509.8 | 0.0 | 0.00 | ***726.2*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***726.2*** |
| A0103 | Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu | 2,021.0 | 1,838.6 | 0.0 | 0.00 | ***3,859.7*** | 3,400.0 | 0.0 | 0.0 | ***3,400.0*** | ***7,259.7*** |
| **A02** | ***Ofisi ya Baraza la Mapinduzi*** | **1,330.7** | 1,080.0 | 0.0 | 0.00 | ***2,410.7*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***2,410.7*** |
| A0201 | Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya BLM. | 0.0 | 515.5 | 0.0 | 0.00 | ***515.5*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***515.5*** |
| A0202 | Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi. | 1,330.7 | 564.5 | 0.0 | 0.00 | ***1,895.2*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***1,895.2*** |
| **A07** | ***Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji-(Kazi na Uwezeshaji)*** | **3,145.4** | 1,993.7 | 2,784.5 | 0.00 | ***7,923.6*** | 4,500.0 | 2,540.6 | 0.0 | ***7,041.0*** | ***14,964.2*** |
| A0702 | Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote | 0.0 | 0.0 | 1,738.4 | 0.00 | ***1,738.4*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***1,738.4*** |
| A0703 | Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. | 1,688.7 | 991.0 | 1,046.1 | 0.00 | ***3,725.8*** | 4,500.0 | 2,540.6 | 0.0 | ***7,041.0*** | ***10,766.4*** |
| A0705 | Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji | 1,456.7 | 1,002.7 | 0.0 | 0.00 | ***2,459.4*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***2,459.4*** |
| **A08** | ***Afisi ya Rais, Kazi, - Uchumi na Uwekezaji-(Uchumi na Uwekezaji)*** | **770.1** | 1,074.3 | 2,887.8 | 0.00 | ***4,732.2*** | 3,500.0 | 0.0 | 0.0 | ***3,500.0*** | ***8,232.2*** |
| A0801 | Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi | 129.1 | 355.0 | 2,887.8 | 0.00 | ***3,371.9*** | 3,500.0 | 0.0 | 0.0 | ***3,500.0*** | ***6,871.9*** |

## MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| Wizara/Taasisi | | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| A0802 | Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji | 641.0 | 719.3 | 0.0 | 0.00 | *1,360.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,360.3* |
| **A09** | ***Taasisi ya Afisi ya Rais ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini*** | **1,532.9** | 715.0 | 0.0 | 0.00 | *2,247.9* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | ***2,247.9*** |
| A0901 | Usimamizi na Uratibu wa Shughuli na Huduma zinazotolewa na Serikali | 0.0 | 556.0 | 0.0 | 0.00 | *556.0* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *556.0* |
| A0902 | Mipango na Uendeshaji ya Taasisi ya Usimaz na Ufuatiliaji wa Shughuli na Huduma zinazotolewa na SMZ | 1,532.9 | 159.0 | 0.0 | 0.00 | *1,691.9* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,691.9* |
| **A10** | ***Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu*** | **631.6** | 568.9 | 0.0 | 0.00 | *1,200.5* | 4,500.0 | 0.0 | 0.0 | *4,500.0* | ***5,700.5*** |
| A1001 | Utunzaji wa Nyaraka na Kumbukumbu kwa Matumizi ya Serikali na Umma | 0.0 | 199.7 | 0.0 | 0.00 | *199.7* | 4,500.0 | 0.0 | 0.0 | *4,500.0* | *4,699.7* |
| A1002 | Utawala na Uendeshaji | 631.6 | 369.2 | 0.0 | 0.00 | *1,000.8* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,000.8* |
| **B01** | ***Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais*** | **2,973.4** | 2,622.1 | 200.0 | 0.00 | *5,795.5* | 3,500.0 | 1,451.0 | 0.0 | *4,951.0* | ***10,746.5*** |
| B0101 | Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi | 422.2 | 218.8 | 0.0 | 0.00 | *641.0* | 3,500.0 | 1,451.0 | 0.0 | *4,951.0* | *5,592.0* |
| B0102 | Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu | 538.5 | 447.7 | 200.0 | 0.00 | *1,186.2* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,186.2* |
| B0103 | Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais | 1,387.6 | 1,381.1 | 0.0 | 0.00 | *2,768.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *2,768.7* |
| B0104 | Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais | 625.2 | 574.5 | 0.0 | 0.00 | *1,199.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,199.7* |
| **B04** | ***Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar*** | **1,030.8** | 543.2 | 0.0 | 0.00 | *1,574.0* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | ***1,574.0*** |
| B0401 | Usimamizi wa Mazingira | 0.0 | 111.3 | 0.0 | 0.00 | *111.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *111.3* |
| B0402 | Utawala na Uendeshaji wa Ofisi | 1,030.8 | 431.9 | 0.0 | 0.00 | *1,462.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,462.7* |
| **C01** | ***Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais*** | **4,550.8** | 3,675.8 | 19,870.6 | 210.81 | *28,308.0* | 100.0 | 2,902.0 | 14,644.0 | *17,646.0* | ***45,954.5*** |

## MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| Wizara/Taasisi | | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| C0101 | Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais | 1,111.1 | 520.1 | 0.0 | 0.00 | *1,631.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,631.3* |
| C0102 | Uratibu wa shughuli za Serikali | 1,424.1 | 2,161.9 | 19,870.6 | 210.81 | *23,667.4* | 100.0 | 2,902.0 | 14,644.0 | *17,646.0* | *41,313.9* |
| C0104 | Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya makamo wa Pili wa Rais | 2,015.6 | 993.8 | 0.0 | 0.00 | *3,009.4* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *3,009.4* |
| **C02** | ***Baraza la Wawakilishi*** | **10,283.3** | 15,717.0 | 0.0 | 0.00 | *26,000.2* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | **26,000.2** |
| C0201 | Kutunga sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali | 0.0 | 8,695.1 | 0.0 | 0.00 | *8,695.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *8,695.1* |
| C0202 | Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | 10,283.3 | 7,021.8 | 0.0 | 0.00 | *17,305.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *17,305.1* |
| **C03** | ***Tume ya Uchaguzi Zanzibar*** | **2,878.1** | 483.4 | 0.0 | 0.00 | *3,361.5* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | **3,361.5** |
| C0302 | Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi Zanzibar | 2,878.1 | 483.4 | 0.0 | 0.00 | *3,361.5* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *3,361.5* |
| **C04** | ***Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar*** | **862.5** | 885.2 | 0.0 | 0.00 | *1,747.7* | 1,500.0 | 0.0 | 0.0 | *1,500.0* | **3,247.7** |
| C0401 | Udhibiti wa Dawa za Kulevya | 0.0 | 377.2 | 0.0 | 0.00 | *377.2* | 1,500.0 | 0.0 | 0.0 | *1,500.0* | *1,877.2* |
| C0402 | Utawala na Rasilimali watu wa ZDCEA | 862.5 | 508.0 | 0.0 | 0.00 | *1,370.5* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,370.5* |
| **C05** | ***Tume ya Ukimwi Zanzibar*** | **666.1** | 517.3 | 0.0 | 26.83 | *1,210.2* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | **1,210.2** |
| C0501 | Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI | 0.0 | 87.9 | 0.0 | 26.83 | *114.8* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *114.8* |
| C0502 | Uratibu na uendeshaji wa Tume ya UKIMWI | 666.1 | 429.4 | 0.0 | 0.00 | *1,095.5* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,095.5* |
| **D01** | ***Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ*** | **2,169.9** | 3,628.7 | 137.6 | 0.00 | *5,936.2* | 28,000.0 | 0.0 | 0.0 | *28,000.0* | **33,936.2** |
| D0101 | Uratibu wa Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa | 209.6 | 282.1 | 0.0 | 0.00 | *491.7* | 3,000.0 | 0.0 | 0.0 | *3,000.0* | *3,491.7* |
| D0102 | Uratibu na Usimamizi wa Idara Maalum | 0.0 | 660.0 | 137.6 | 0.00 | *797.6* | 25,000.0 | 0.0 | 0.0 | *25,000.0* | *25,797.6* |
| D0104 | Uendeshaji na Uratibu wa ORTMSMIM | 1,960.3 | 2,686.6 | 0.0 | 0.00 | *4,646.9* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *4,646.9* |

# MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| Wizara/Taasisi | | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| **D02** | ***Jeshi la Kujenga Uchumi*** | **29,798.1** | 6,400.0 | 479.4 | 0.00 | *36,677.5* | 3,000.0 | 0.0 | 0.0 | ***3,000.0*** | ***39,677.5*** |
| D0201 | Mafunzo kwa Vijana na Uzalishaji Mali | 0.0 | 3,837.3 | 0.0 | 0.00 | *3,837.3* | 3,000.0 | 0.0 | 0.0 | ***3,000.0*** | ***6,837.3*** |
| D0202 | Utawala na Uendeshaji wa JKU | 29,798.1 | 2,562.7 | 479.4 | 0.00 | *32,840.2* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***32,840.2*** |
| **D03** | ***Chuo cha Mafunzo*** | **19,960.4** | 3,934.3 | 0.0 | 0.00 | *23,894.7* | 1,500.0 | 0.0 | 0.0 | ***1,500.0*** | ***25,394.7*** |
| D0301 | Urekebishaji Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo | 0.0 | 1,590.2 | 0.0 | 0.00 | *1,590.2* | 1,500.0 | 0.0 | 0.0 | ***1,500.0*** | ***3,090.2*** |
| D0302 | Utawala na Uendeshaji | 19,960.4 | 2,344.1 | 0.0 | 0.00 | *22,304.5* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***22,304.5*** |
| **D04** | ***Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo*** | **31,384.4** | 3,735.9 | 0.0 | 0.00 | *35,120.3* | 2,500.0 | 0.0 | 0.0 | ***2,500.0*** | ***37,620.3*** |
| D0401 | Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo | 0.0 | 1,826.5 | 0.0 | 0.00 | *1,826.5* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***1,826.5*** |
| D0402 | Uendeshaji na Uratibu wa KIkosi maalum cha Kuzuia Magendo | 31,384.4 | 1,909.4 | 0.0 | 0.00 | *33,293.8* | 2,500.0 | 0.0 | 0.0 | ***2,500.0*** | ***35,793.8*** |
| **D05** | ***Kikosi cha Zimamoto na Uokozi*** | **14,312.6** | 2,012.4 | 0.0 | 0.00 | *16,325.0* | 3,500.0 | 0.0 | 0.0 | ***3,500.0*** | ***19,825.0*** |
| D0501 | Uokozi na Uzimaji moto | 0.0 | 769.0 | 0.0 | 0.00 | *769.0* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***769.0*** |
| D0502 | Utawala na Uendeshaji wa KZU | 14,312.6 | 1,243.4 | 0.0 | 0.00 | *15,556.0* | 3,500.0 | 0.0 | 0.0 | ***3,500.0*** | ***19,056.0*** |
| **D06** | ***Kikosi cha Valantia*** | **19,524.8** | 2,228.8 | 0.0 | 0.00 | *21,753.6* | 1,500.0 | 0.0 | 0.0 | ***1,500.0*** | ***23,253.6*** |
| D0601 | wa Nchi, Raia na Mali zao. | 0.0 | 1,674.5 | 0.0 | 0.00 | *1,674.5* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***1,674.5*** |
| D0602 | Uendeshaji na Utawala wa Kikosi cha Valantia | 19,524.8 | 554.3 | 0.0 | 0.00 | *20,079.1* | 1,500.0 | 0.0 | 0.0 | ***1,500.0*** | ***21,579.1*** |
| **D07** | ***Mkoa wa Mjini Magharibi*** | **2,358.0** | 1,062.3 | 8,530.8 | 0.00 | *11,951.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***11,951.1*** |
| D0701 | Kusimamia shughuli za Serikali Katika Mkoa | 0.0 | 415.7 | 0.0 | 0.00 | *415.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***415.7*** |
| D0702 | Uendeshaji na Utawala wa Mkoa, Wilaya na Shehia | 2,358.0 | 646.6 | 0.0 | 0.00 | *3,004.6* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***3,004.6*** |
| D0703 | Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa | 0.0 | 0.0 | 8,530.8 | 0.00 | *8,530.8* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***8,530.8*** |
| **D08** | ***Mkoa wa Kusini Unguja*** | **2,902.5** | 286.4 | 1,936.9 | 0.00 | *5,125.8* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***5,125.8*** |

## MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| Wizara/Taasisi | | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| D0801 | Kuratibu Utekelezaji wa Shughuli za Serikali katika Mkoa | 0.0 | 99.2 | 0.0 | 0.00 | *99.2* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *99.2* |
| D0802 | Uendeshaji na Utawala wa Mkoa wa Kusini Unguja | 2,902.5 | 187.2 | 0.0 | 0.00 | *3,089.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *3,089.7* |
| D0803 | Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa | 0.0 | 0.0 | 1,936.9 | 0.00 | *1,936.9* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,936.9* |
| **D09** | ***Mkoa wa Kaskazini Unguja*** | **1,956.4** | 525.1 | 2,269.8 | 0.00 | *4,751.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *4,751.3* |
| D0901 | Kuimarisha Shughuli za Serikali katika Mkoa | 0.0 | 153.1 | 0.0 | 0.00 | *153.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *153.1* |
| D0902 | Utawala na Uendeshaji wa Mkoa, Wilaya na Shehia | 1,956.4 | 372.0 | 0.0 | 0.00 | *2,328.4* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *2,328.4* |
| D0903 | Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa | 0.0 | 0.0 | 2,269.8 | 0.00 | *2,269.8* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *2,269.8* |
| **D10** | ***Mkoa wa Kusini Pemba*** | **1,428.2** | 622.6 | 3,127.8 | 0.00 | *5,178.6* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *5,178.6* |
| D1001 | Kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa | 0.0 | 124.9 | 0.0 | 0.00 | *124.9* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *124.9* |
| D1003 | Uendeshaji na Utawala wa Mkoa, Wilaya na Shehia | 1,428.2 | 497.7 | 0.0 | 0.00 | *1,925.9* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,925.9* |
| D1004 | Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa | 0.0 | 0.0 | 3,127.8 | 0.00 | *3,127.8* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *3,127.8* |
| **D11** | ***Mkoa wa Kaskazini Pemba*** | **1,462.8** | 581.7 | 2,338.2 | 0.00 | *4,382.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *4,382.7* |
| D1101 | Kusimamia shughuli za Serikali katika Mkoa | 0.0 | 213.4 | 0.0 | 0.00 | *213.4* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *213.4* |
| D1103 | Uendeshaji na Utawala wa Mkoa, Wilaya na Shehia | 1,462.8 | 368.3 | 0.0 | 0.00 | *1,831.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,831.1* |
| D1104 | Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa | 0.0 | 0.0 | 2,338.2 | 0.00 | *2,338.2* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *2,338.2* |
| **D12** | ***Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii*** | **2,635.3** | 1,561.5 | 0.0 | 0.00 | *4,196.8* | 950.0 | 0.0 | 0.0 | *950.0* | *5,146.8* |
| D1201 | Kusajili Vizazi,Vifo na Kadi za Utambulisho | 0.0 | 606.5 | 0.0 | 0.00 | *606.5* | 950.0 | 0.0 | 0.0 | *950.0* | *1,556.5* |

## MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| Wizara/Taasisi | | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| D1202 | Utumishi na Uendeshaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 2,635.3 | 955.0 | 0.0 | 0.00 | *3,590.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *3,590.3* |
| **E04** | ***Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali*** | **4,683.9** | 1,808.5 | 0.0 | 0.00 | *6,492.4* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *6,492.4* |
| E0401 | Ukaguzi wa Fedha na Rasilimali za Umma | 1,974.6 | 399.1 | 0.0 | 0.00 | *2,373.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *2,373.7* |
| E0402 | Huduma za Ukaguzi wa Fedha Kiutawala na Uendeshaji | 2,709.3 | 1,409.4 | 0.0 | 0.00 | *4,118.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *4,118.7* |
| **E05** | ***Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar*** | **3,136.2** | 1,158.4 | 0.0 | 0.00 | *4,294.6* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *4,294.6* |
| E0501 | Kupunguza Matendo ya Rushwa na Uhujumu Uchumi | 0.0 | 365.9 | 0.0 | 0.00 | *365.9* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *365.9* |
| E0502 | Utawala na Uendeshaji wa Mamlaka ya kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi | 3,136.2 | 792.5 | 0.0 | 0.00 | *3,928.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *3,928.7* |
| **E07** | ***Kamisheni ya Utumishi wa Umma*** | **728.9** | 520.9 | 0.0 | 0.00 | *1,249.8* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,249.8* |
| E0701 | Usimamizi wa Utumishi wa Umma | 0.0 | 94.6 | 0.0 | 0.00 | *94.6* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *94.6* |
| E0702 | Utawala na Uendeshaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma | 728.9 | 426.3 | 0.0 | 0.00 | *1,155.2* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,155.2* |
| **E08** | ***Tume ya Utumishi Serikalini*** | **458.6** | 409.1 | 0.0 | 0.00 | *867.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *867.7* |
| E0801 | Usimamizi wa Watumishi Serikalini | 0.0 | 230.4 | 0.0 | 0.00 | *230.4* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *230.4* |
| E0802 | Utawala na Uendeshaji wa Huduma za Watumishi | 458.6 | 178.7 | 0.0 | 0.00 | *637.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *637.3* |
| **F01** | ***Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango*** | **90,636.3** | 11,555.7 | 39,588.8 | 87.22 | *141,868.0* | 218,285.1 | 4,118.9 | 24,501.0 | *246,905.0* | *388,773.2* |
| F0101 | Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma | 87,422.2 | 1,871.9 | 36,972.3 | 87.22 | *126,353.7* | 0.0 | 350.0 | 0.0 | *350.0* | *126,703.7* |
| F0102 | Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma | 552.1 | 3,125.5 | 2,616.5 | 0.00 | *6,294.0* | 74,122.0 | 0.0 | 0.0 | *74,122.0* | *80,416.0* |
| F0104 | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango | 2,661.9 | 6,558.3 | 0.0 | 0.00 | *9,220.2* | 144,163.1 | 3,768.9 | 24,501.0 | *172,433.0* | *181,653.5* |

## MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| Wizara/Taasisi | | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| **F02** | ***Mfuko Mkuu wa Serikali.*** | **2,449.4** | 256,000.0 | 0.0 | 0.00 | ***258,449.4*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***258,449.4*** |
| F0201 | Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | 2,449.4 | 256,000.0 | 0.0 | 0.00 | ***258,449.4*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***258,449.4*** |
| **F03** | ***Tume ya Mipango*** | **1,809.2** | 2,343.9 | 0.0 | 1,013.94 | ***5,167.0*** | 5,500.0 | 500.0 | 0.0 | ***6,000.0*** | ***11,167.0*** |
| F0301 | Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda Kazi | 689.0 | 514.4 | 0.0 | 556.34 | ***1,759.8*** | 5,500.0 | 500.0 | 0.0 | ***6,000.0*** | ***7,759.8*** |
| F0302 | Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Tafiti | 391.7 | 521.0 | 0.0 | 457.60 | ***1,370.3*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***1,370.3*** |
| F0303 | Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Mipango | 728.5 | 1,308.4 | 0.0 | 0.00 | ***2,036.9*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***2,036.9*** |
| **F04** | ***Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali*** | **2,220.0** | 1,557.6 | 0.0 | 61.46 | ***3,839.1*** | 0.0 | 0.0 | 4,427.0 | ***4,427.0*** | ***8,266.5*** |
| F0401 | Kuendeleza na Kuratibu Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii | 1,337.4 | 669.6 | 0.0 | 0.00 | ***2,007.1*** | 0.0 | 0.0 | 3,969.0 | ***3,969.0*** | ***5,975.8*** |
| F0402 | Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | 882.6 | 888.0 | 0.0 | 61.46 | ***1,832.0*** | 0.0 | 0.0 | 459.0 | ***459.0*** | ***2,290.6*** |
| **F05** | ***Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali*** | **8,929.5** | 2,212.5 | 0.0 | 0.00 | ***11,142.0*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***11,142.0*** |
| F0501 | Usimamizi wa Hazina | 0.0 | 664.3 | 0.0 | 0.00 | ***664.3*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***664.3*** |
| F0502 | Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 8,929.5 | 1,548.2 | 0.0 | 0.00 | ***10,477.7*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***10,477.7*** |
| **F06** | ***Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali*** | **3,654.9** | 1,427.0 | 0.0 | 0.00 | ***5,081.9*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***5,081.9*** |
| F0601 | Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani Serikalini | 0.0 | 210.6 | 0.0 | 0.00 | ***210.6*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***210.6*** |
| F0602 | Utawala na Uendeshaji | 3,654.9 | 1,216.4 | 0.0 | 0.00 | ***4,871.3*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***4,871.3*** |
| **G01** | ***Afisi ya Rais,Katiba, Sheria,Utumishi na utawala bora*** | **3,350.7** | 2,132.7 | 2,757.5 | 0.00 | ***8,240.9*** | 1,000.0 | 1,343.2 | 0.0 | ***2,343.0*** | ***10,584.1*** |
| G0102 | Usimamizi wa Masuala ya Sheria | 108.3 | 115.0 | 0.0 | 0.00 | ***223.3*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***223.3*** |
| G0103 | Usimamizi wa Utawala Bora | 216.6 | 100.0 | 0.0 | 0.00 | ***316.6*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***316.6*** |
| G0105 | Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais,Katiba,Sheria ,Utumishi na Utawala Bora | 2,170.8 | 1,424.0 | 2,757.5 | 0.00 | ***6,352.3*** | 1,000.0 | 1,343.2 | 0.0 | ***2,343.0*** | ***8,695.5*** |

## MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| Wizara/Taasisi | | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| G0106 | Usimamizi wa rasilimali watu na Utumishi wa Umma | 855.0 | 493.7 | 0.0 | 0.00 | *1,348.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,348.7* |
| **G02** | ***Mahkama Kuu Zanzibar*** | **7,462.9** | 3,767.6 | 1,681.0 | 0.00 | ***12,911.5*** | 27,000.0 | 0.0 | 0.0 | ***27,000.0*** | ***39,911.5*** |
| G0201 | Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki | 0.0 | 1,050.7 | 1,681.0 | 0.00 | *2,731.7* | 27,000.0 | 0.0 | 0.0 | *27,000.0* | *29,731.7* |
| G0202 | Uendeshaji na Uratibu wa Mahkama Kuu | 7,462.9 | 2,716.9 | 0.0 | 0.00 | *10,179.8* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *10,179.8* |
| **G03** | ***Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar*** | **2,379.4** | 988.8 | 0.0 | 0.00 | ***3,368.2*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***3,368.2*** |
| G0301 | Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria | 0.0 | 171.2 | 0.0 | 0.00 | *171.2* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *171.2* |
| G0302 | Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu | 2,379.4 | 817.6 | 0.0 | 0.00 | *3,197.0* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *3,197.0* |
| **G04** | ***Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka*** | **2,621.3** | 1,000.4 | 158.7 | 0.00 | ***3,780.4*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***3,780.4*** |
| G0401 | Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Jinai | 0.0 | 294.3 | 0.0 | 0.00 | *294.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *294.3* |
| G0402 | Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | 2,621.3 | 706.1 | 158.7 | 0.00 | *3,486.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *3,486.1* |
| **G05** | ***Tume ya Kurekebisha Sheria*** | **827.4** | 1,039.3 | 0.0 | 0.00 | ***1,866.7*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***1,866.7*** |
| G0501 | Kufanya Mapitio ya Sheria | 0.0 | 482.0 | 0.0 | 0.00 | *482.0* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *482.0* |
| G0502 | Utawala na Uratibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria | 827.4 | 557.3 | 0.0 | 0.00 | *1,384.7* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,384.7* |
| **G12** | ***Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana*** | **1,347.6** | 582.5 | 0.0 | 0.00 | ***1,930.1*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***1,930.1*** |
| G1201 | Usimamizi wa Haki na Uwezeshaji Kishariah | 0.0 | 170.6 | 0.0 | 0.00 | *170.6* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *170.6* |
| G1202 | Utawala na Uendeshaji wa Ofisi | 1,347.6 | 411.9 | 0.0 | 0.00 | *1,759.5* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,759.5* |
| **G13** | ***Wakala wa Serikali Mtandao*** | **1,249.7** | 1,958.9 | 0.0 | 0.00 | ***3,208.6*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***3,208.6*** |
| G1301 | Huduma za Serikali Mtandao | 708.4 | 1,088.9 | 0.0 | 0.00 | *1,797.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,797.3* |
| G1302 | Uendeshaji wa Serikali Mtandao | 541.3 | 870.0 | 0.0 | 0.00 | *1,411.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,411.3* |
| **G14** | ***Afisi ya Mufti Mkuu*** | **1,155.1** | 667.0 | 0.0 | 0.00 | ***1,822.1*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***1,822.1*** |
| G1401 | Usimamizi wa mambo ya Kiislam | 0.0 | 295.2 | 0.0 | 0.00 | *295.2* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *295.2* |

## MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| Wizara/Taasisi | | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| G1402 | Utawala na Uendeshaji | 1,155.1 | 371.8 | 0.0 | 0.00 | *1,526.9* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,526.9* |
| **G15** | ***Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma*** | **640.8** | 660.3 | 0.0 | 0.00 | *1,301.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,301.1* |
| G1501 | Maadili ya Viongozi wa Umma | 0.0 | 385.1 | 0.0 | 0.00 | *385.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *385.1* |
| G1502 | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 640.8 | 275.2 | 0.0 | 0.00 | *916.0* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *916.0* |
| **H01** | ***Wizara ya Afya*** | **60,013.8** | 56,013.8 | 5,062.6 | 2,613.25 | *123,703.5* | 53,050.0 | 10,836.3 | 1,790.0 | *65,676.0* | *189,379.4* |
| H0101 | Kinga na Elimu ya Afya | 22,225.9 | 4,329.1 | 0.0 | 1,457.18 | *28,012.1* | 2,050.0 | 6,836.3 | 0.0 | *8,886.0* | *36,898.4* |
| H0102 | Huduma za Tiba | 9,261.5 | 46,351.3 | 4,581.1 | 64.35 | *60,258.3* | 51,000.0 | 4,000.0 | 1,790.0 | *56,790.0* | *117,047.9* |
| H0103 | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya | 28,526.5 | 5,333.4 | 481.5 | 1,091.72 | *35,433.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *35,433.1* |
| **H02** | ***Hospitali ya Mnazi Mmoja*** | **24,372.4** | 14,274.4 | 0.0 | 0.00 | *38,646.8* | 1,125.2 | 0.0 | 10,000.0 | *11,125.0* | *49,772.0* |
| H0201 | Huduma za Uchunguzi na Matibabu | 0.0 | 11,374.8 | 0.0 | 0.00 | *11,374.8* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *11,374.8* |
| H0202 | Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazimmoja | 24,372.4 | 2,899.6 | 0.0 | 0.00 | *27,272.0* | 1,125.2 | 0.0 | 10,000.0 | *11,125.0* | *38,397.2* |
| **H04** | ***Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto*** | **3,170.0** | 4,000.0 | 0.0 | 580.99 | *7,751.0* | 1,500.0 | 636.3 | 0.0 | *2,136.0* | *9,887.3* |
| H0401 | Hifadhi ya Jamii | 0.0 | 1,046.1 | 0.0 | 48.56 | *1,094.7* | 1,500.0 | 0.0 | 0.0 | *1,500.0* | *2,594.7* |
| H0402 | Utawala na Uendeshaji | 3,170.0 | 2,478.9 | 0.0 | 0.00 | *5,648.9* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *5,648.9* |
| H0403 | Maendeleo ya Jamii na Jinsia | 0.0 | 475.0 | 0.0 | 532.43 | *1,007.4* | 0.0 | 636.3 | 0.0 | *636.0* | *1,643.8* |
| **J03** | ***Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo*** | **5,455.2** | 2,103.2 | 10,040.6 | 62.93 | *17,661.9* | 33,000.0 | 1,278.1 | 0.0 | *34,278.0* | *51,940.0* |
| J0301 | Maendeleo ya Habari ,Utangazaji na Uchapaji | 698.1 | 200.2 | 8,714.0 | 0.00 | *9,612.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *9,612.3* |
| J0302 | Maendeleo ya Vijana | 215.3 | 104.1 | 246.3 | 62.93 | *628.6* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *628.6* |
| J0303 | Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo | 2,221.0 | 576.8 | 1,080.3 | 0.00 | *3,878.1* | 33,000.0 | 1,278.1 | 0.0 | *34,278.0* | *38,156.2* |
| J0304 | Utawala na Uendeshaji | 2,320.9 | 1,222.1 | 0.0 | 0.00 | *3,542.9* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *3,542.9* |

## MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| Wizara/Taasisi | | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| **J04** | ***Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale*** | **3,289.7** | 1,573.6 | 1,150.2 | 971.40 | ***6,984.9*** | 7,000.0 | 0.0 | 0.0 | ***7,000.0*** | ***13,984.9*** |
| J0401 | Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii | 246.9 | 224.4 | 0.0 | 187.42 | ***658.7*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***658.7*** |
| J0402 | Maendeleo ya Makumbusho , Mambo ya kale na uhifadhi wa Mji Mkongwe | 1,285.4 | 408.9 | 1,150.2 | 241.09 | ***3,085.6*** | 7,000.0 | 0.0 | 0.0 | ***7,000.0*** | ***10,085.6*** |
| J0403 | Utawala na Uendeshaji | 1,757.4 | 940.3 | 0.0 | 542.89 | ***3,240.6*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***3,240.6*** |
| **K01** | ***Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali*** | **190,927.2** | 35,743.1 | 49,558.3 | 0.00 | ***276,228.6*** | 98,970.7 | 31,570.3 | 50,530.0 | ***181,071.0*** | ***457,299.6*** |
| K0101 | Elimu ya Maandalizi na Msingi | 85,494.1 | 10,636.3 | 0.0 | 0.00 | ***96,130.4*** | 16,248.3 | 6,079.4 | 14,027.0 | ***36,355.0*** | ***132,485.2*** |
| K0102 | Elimu ya Sekondari | 93,089.0 | 13,676.3 | 0.0 | 0.00 | ***106,765.3*** | 54,694.4 | 2,054.0 | 26,503.0 | ***83,252.0*** | ***190,016.9*** |
| K0103 | Elimu ya Juu | 842.6 | 390.0 | 30,223.5 | 0.00 | ***31,456.1*** | 22,268.0 | 0.0 | 5,000.0 | ***27,268.0*** | ***58,724.1*** |
| K0104 | Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali | 885.5 | 528.0 | 8,630.7 | 0.00 | ***10,044.2*** | 5,760.0 | 19,224.5 | 2,000.0 | ***26,984.0*** | ***37,028.6*** |
| K0105 | Ubora wa Elimu | 813.8 | 977.9 | 10,704.1 | 0.00 | ***12,495.8*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***12,495.8*** |
| K0106 | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Elimu | 9,802.1 | 9,534.7 | 0.0 | 0.00 | ***19,336.8*** | 0.0 | 4,212.4 | 3,000.0 | ***7,212.0*** | ***26,548.9*** |
| **L01** | ***Wizara ya Kilimo,Umwagiliaji,Maliasili na Mifugo*** | **16,886.8** | 3,574.0 | 9,731.2 | 0.00 | ***30,192.0*** | 25,000.0 | 12,323.8 | 31,201.0 | ***68,524.0*** | ***98,716.4*** |
| L0101 | Maendeleo ya Kilimo | 5,483.0 | 1,312.9 | 7,735.0 | 0.00 | ***14,530.9*** | 23,000.0 | 11,809.8 | 31,201.0 | ***66,010.0*** | ***80,541.3*** |
| L0102 | Maendeleo ya Rasilimali za Misitu | 2,512.1 | 430.5 | 0.0 | 0.00 | ***2,942.6*** | 0.0 | 514.0 | 0.0 | ***514.0*** | ***3,456.6*** |
| L0103 | Maendeleo ya Mifugo | 2,751.8 | 552.0 | 1,996.2 | 0.00 | ***5,300.0*** | 2,000.0 | 0.0 | 0.0 | ***2,000.0*** | ***7,300.0*** |
| L0105 | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo | 6,139.9 | 1,278.6 | 0.0 | 0.00 | ***7,418.5*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***7,418.5*** |
| **L02** | ***Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi*** | **3,814.3** | 2,452.4 | 3,046.3 | 0.00 | ***9,313.0*** | 35,500.0 | 16,827.0 | 19,421.0 | ***71,748.0*** | ***81,061.0*** |
| L0201 | Maendeleo ya Uchumi wa Buluu | 167.1 | 602.1 | 2,378.2 | 0.00 | ***3,147.4*** | 8,000.0 | 6,000.0 | 0.0 | ***14,000.0*** | ***17,147.4*** |
| L0202 | Maendeleo ya Uvuvi | 1,886.5 | 711.2 | 668.1 | 0.00 | ***3,265.8*** | 27,500.0 | 10,827.0 | 15,921.0 | ***54,248.0*** | ***57,513.8*** |
| L0203 | Uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 1,760.7 | 1,139.1 | 0.0 | 0.00 | ***2,899.8*** | 0.0 | 0.0 | 3,500.0 | ***3,500.0*** | ***6,399.8*** |
| **N02** | ***Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi*** | **4,079.5** | 1,455.6 | 1,488.8 | 0.00 | ***7,023.9*** | 0.0 | 0.0 | 0.0 | ***0.0*** | ***7,023.9*** |

## MAKISIO YA BAJETI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| Wizara/Taasisi | | Matumizi ya Kawaida '000,000 | | | | | Matumizi ya Maendeleo '000,000 | | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Gharama za OC | Ruzuku | Ruzuku za Nje | Jumla | SMZ | Misaada ya Nje | Mikopo ya Nje | Jumla | |
| N0201 | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 3,736.9 | 1,210.6 | 0.0 | 0.00 | *4,947.5* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *4,947.5* |
| N0202 | Usimamizi wa Ardhi | 342.6 | 245.0 | 213.7 | 0.00 | *801.3* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *801.3* |
| N0203 | Maendeleo ya Makaazi | 0.0 | 0.0 | 1,275.1 | 0.00 | *1,275.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *1,275.1* |
| **N03** | ***Wizara ya Maji, Nishati na Madini*** | **2,407.6** | 8,014.1 | 5,863.5 | 0.00 | *16,285.2* | 48,705.0 | 13,227.1 | 48,729.0 | *110,661.0* | *126,945.9* |
| N0301 | Usimamizi wa Huduma za Maji. | 250.0 | 139.8 | 5,863.5 | 0.00 | *6,253.3* | 24,505.0 | 13,159.5 | 39,850.0 | *77,515.0* | *83,768.1* |
| N0302 | Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini | 722.3 | 7,160.0 | 0.0 | 0.00 | *7,882.3* | 24,200.0 | 67.6 | 8,878.0 | *33,146.0* | *41,028.3* |
| N0303 | Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM | 1,435.3 | 714.3 | 0.0 | 0.00 | *2,149.6* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *2,149.6* |
| **N04** | ***Kamisheni ya Ardhi*** | **3,040.7** | 1,621.5 | 773.1 | 0.00 | *5,435.3* | 4,550.0 | 0.0 | 0.0 | *4,550.0* | *9,985.3* |
| N0401 | Utawala na Uendeshaji wa Kamisheni ya Ardhi | 3,040.7 | 968.3 | 0.0 | 0.00 | *4,009.1* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *4,009.1* |
| N0402 | Utawala na Usimamizi wa Ardhi | 0.0 | 653.2 | 773.1 | 0.00 | *1,426.2* | 4,550.0 | 0.0 | 0.0 | *4,550.0* | *5,976.2* |
| **P01** | ***Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi*** | **2,751.3** | 2,630.7 | 6,661.7 | 0.00 | *12,043.7* | 235,447.0 | 0.0 | 324,000.0 | *559,447.0* | *571,490.7* |
| P0101 | Programu ya Usafirishaji | 0.0 | 0.0 | 6,661.7 | 0.00 | *6,661.7* | 229,547.0 | 0.0 | 324,000.0 | *553,547.0* | *560,208.7* |
| P0103 | Programu ya Technolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) | 299.1 | 400.7 | 0.0 | 0.00 | *699.8* | 5,900.0 | 0.0 | 0.0 | *5,900.0* | *6,599.8* |
| P0104 | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | 2,452.2 | 2,230.0 | 0.0 | 0.00 | *4,682.2* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *4,682.2* |
| **R01** | ***Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda*** | **4,304.1** | 1,646.5 | 1,584.4 | 0.00 | *7,535.0* | 28,417.0 | 0.0 | 0.0 | *28,417.0* | *35,952.0* |
| R0101 | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara | 2,806.6 | 1,246.8 | 0.0 | 0.00 | *4,053.4* | 0.0 | 0.0 | 0.0 | *0.0* | *4,053.4* |
| R0102 | Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali | 197.8 | 195.3 | 0.0 | 0.00 | *393.0* | 26,012.0 | 0.0 | 0.0 | *26,012.0* | *26,405.0* |
| R0103 | Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara | 1,299.7 | 204.4 | 1,584.4 | 0.00 | *3,088.5* | 2,405.0 | 0.0 | 0.0 | *2,405.0* | *5,493.5* |
| | **JUMLA KUU** | **631,403.5** | **487,313.6** | **183,710.1** | **5,628.83** | **1,308,056.1** | **886,000.0** | **99,554.6** | **529,243.0** | ***1,514,798.0*** | **2,822,853.7** |

**IMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 21 Juni, 2023.

.................................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***